

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BARAZA LA MITIHANI
MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A**

610

UALIMU

Muda: Saa 3

Jumanne, 05 Mei 2015 asubuhi

Maelekezo

1. Karatasi hii ina sehemu A, B, C, D na E.
2. Jibu maswali **yote** katika sehemu A na swali **moja (1)** kutoka katika kila sehemu B, C, D na E.
3. Sehemu A ina alama 40, sehemu B, C, D na E zina alama 15 kila moja.
4. Simu za mkononi **haziruhusiwi** ndani ya chumba cha mtihani.
5. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

SEHEMU A (Alama 40)

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

1. Bainisha mambo manne yanayoweza kuathiri ukuaji wa mtoto katika hatua za awali **kabla** hajazaliwa.
2. Orodhesha sifa nne za malengo mahsusini katika ufundishaji na ujifunzaji.
3. Kwa kutumia hoja nne eleza kwa kifupi umuhimu wa mafunzo kazini.
4. (a) Mfiko wa alama ni nini? Mfiko wa alama za watahiniwa unapokuwa mdogo katika mtihani inamaanisha nini?
(b) Tofautisha kati ya variansi na achano sanifu.
5. Orodhesha mambo manne yanayopaswa kuzingatiwa ili tendo la kuhawilisha **mafunzo liweze** kutokea.
6. Andika kwa kifupi changamoto nne ambazo mwalimu anaweza kukutana **nazo wakati wa kufundisha** iwapo hatafanya matayarisho ya kutosha.
7. Taja mambo manne yanayowafanya Wanasaikolojia kutumia wanyama katika majaribio badala ya binadamu.
8. Bainisha mambo manne ambayo mwanafunzi mtu mzima huvutiwa nayo na kumfanya awe na ari ya kujifunza kusoma na kuandika.
9. Orodhesha sababu nne za kuwepo kitengo cha ushauri na unasihi katika shule za msingi.
10. Eleza kwa kifupi manufaa manne ya kuchanganua swalii.

SEHEMU B: SAIKOLOJIA YA ELIMU (Alama 15)

Jibu swali **moja (1)** kutoka sehemu hii.

11. Mwalimu hana budi kufahamu mwenendo wa mtoto aliyevia akili. Eleza tabia sita za mtoto aliyevia akili.
12. Eleza kwa ufasaha mambo sita yanayoweza kumfanya mwanafunzi kusahau mambo aliyojifunza.

SEHEMU C: MITAALA NA UFUNDISHAJI (Alama 15)

Jibu swali **moja (1)** kutoka sehemu hii.

13. “Kuwaadhibu wanafunzi kwa kutumia fimbo si njia sahihi ya kuweza kulimudu darasa”. Thibitisha kauli hii kwa kutumia hoja sita.
14. Wanafunzi wa Darasa la Sita wa Shule ya Msingi Azimio mkoani Morogoro wameomba kufanya ziara ya mafunzo katika mbuga ya wanyama ya Mikumi. Andika matayarisho sita muhimu kama mwalimu wa Darasa ili kufanikisha ziara hiyo.

SEHEMU D: UTAFITI WA KIELIMU, UPIMAJI NA TATHMINI (Alama 15)

Jibu swali **moja (1)** kutoka sehemu hii.

15. Kwa kutumia hoja sita, jadili umuhimu wa tathmini katika elimu.
16. Bainisha vipengele muhimu wakati wa kuandika ripoti ya utafiti wa kielimu kwa kuzingatia sura ya kwanza mpaka ya sita.

SEHEMU E: MISINGI YA ELIMU (Alama 15)

Jibu swali **moja (1)** kutoka sehemu hii.

17. Jadili mafanikio na changamoto za elimu nchini Tanzania katika karne ya ishirini na moja. Tumia hoja sita, tatu kila upande.
18. (a) Eleza dhana ya Kamati ya Shule.
(b) Kwa kutumia hoja sita, eleza umuhimu wa Kamati ya Shule.